Toleo Na. 002

# JARIDA LA USHIRIKA

Jarida la Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania APRILI - JUNI 2020



"USHIRIKA - PAMOJA TUJENGE UCHUMI"

# DIRA

KuwaTaasisi inayoongoza Afrika katika kuendelezaVyama vya Ushirika vya kisasa na vyenye uwezo kiuchumi, vinavyokidhi viwango vya kimataifa pamoja na mahitaji ya Sekta ya Ushirika.

# DHIMA

Kutoa huduma za Uhamasishaji na Usimamizi zilizo bora na zenye ufanisi ili kuwezesha kuwa naVyama vya Ushirika vya kisasa na vilivyo imara kiuchumi nchini Tanzania.

# MAJUKUMU YA TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA

Majukumu makuu yaTume ya Maendeleo ya Ushirika ni kusimamia na kuhamasisha maendeleo ya sekta ya ushirika kwa kutekeleza yafuatayo:-

i. Kuandikisha na kufuta vyama vya ushirika;
ii. Kusimamia na kudhibiti vyama vya ushirika;
iii. Kutunza na kuboresha rejista ya vyama vya ushirika;
iv. Kutatua migogoro na malalamiko katika vyama vya ushirika;
v. Kuhimiza na kuhamasisha maendeleo endelevu na ya kiuchumi ya vyama vya ushirika;
vi. Kutoa elimu na mafunzo kwa wanachama na watumishi wa vyama vya ushirika kuhusu uendeshaji wa ushirika;
vii. Kukusanya, kuhifadhi na kusambaza takwimu na taarifa za vyama vya ushirika; na
viii. Kufanya tafiti mbalimbali kwa maendeleo ya vyama vya ushirika;

# YALIYOMO

KUTOKA KWA MRAJIS WA VYAMA VYA USHIRIKA NA MTENDAJI MKUU WA TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA……..........................................................................01
WAKULIMA WATAKIWA KUWA NA VITAMBULISHO - WAZIRI HASUNGA............02
NAIBU WAZIRI BASHE ATAKA USHIRIKA KUJIENDESHA KIBIASHARA…….........04
USHIRIKA UJIKITE KATIKA UCHUMI WA VIWANDA- KATIBU MKUU KILIMO …05
UJIO WA SHERIA YA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA KULETA SULUHU YA RIBA KUBWA ZA MIKOPO…..................................................................................................06
USHIRIKA UNAVYOWAKOMBOA WANAWAKE…................................................09
WAKULIMA WAHAMASISHWA KUWEKA AKIBA…................................................11
CHAMA CHA USHIRIKA WA MAZIWA AYALABE-KARATU….................................13
JE, WAJUA WATOA HUDUMA WANAVYOONGEZA KASI YA MAENDELEO YA USHIRIKA? ..............................................................................................................16
DONDOO ZA USHIRIKA...........................................................................………19
IJUE SCCULT (1992) LTD…...................................................................……..20
KATAVI ILIVYODHAMIRIA KUKUZA UCHUMI KUPITIA USHIRIKA……..................23
CHAMA KIKUU CHA USHIRIKA CHA WAKULIMA (LATCU LTD).................................24
HEIFER INTERNATIONAL YATOA GARI NA CANS KWA VYAMA VYA USHIRIKA WA WAFUGAJI MKOANI TANGA…...........................................................................…28
USHIRIKA WA NYUMBA KUWAWEZESHA WANANCHI KUPATA NYUMBA BORA……...............................................................................................................30

# KUTOKA KWA MRAJIS WA VYAMA VYA USHIRIKA NA MTENDAJI MKUU WA TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA



*Dkt. Benson Ndiege*
*Mrajis wa Vyama vya Ushirika na*
*Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika*

**Ndugu Wasomaji,**

Kwanza napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufanikisha utekelezaji wa majukumu yetu mbalimbali ya Ushirika. Nichukue fursa hii kuwakaribisha katika Toleo letu la Pili la Jarida la Ushirika. Toleo lenye mkusanyiko wa habari, Makala na Taarifa zinazohusu Sekta ya Ushirika. Nichukue fursa hii kupongeza juhudi zinazoendelea kufanyika katika Sekta ya Ushirika hususan kuimarisha masoko ya mazao ya Kimkakati kwa kuhamasisha matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi ya Ghala kupitia Vyama vya Ushirika. Katika msimu wa 2019/20, mazao yenye thamani ya Shillingi Trillioni 2.7 yaliuzwa kupitia mfumo wa Ushirika. Mfano; zao la Kakao katika Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya kwa mwaka wa fedha 2017/18 kurudi nyuma, bei kwa kilo ilianzia Shillingi 1,500 hadi 3,500 hadi kufikia tarehe 21.02.2020 bei katika mnada ilipanda hadi kufika Shillingi 5,787 kwa kilo. Katika kuhakikisha huduma bora kwa wanaushirika na Taifa kwa ujumla Tume ya Maendeleo ya Ushirika imeimarisha mfumo wa usimamizi na ukusanyaji wa mapato kwa njia Kielektroniki (GePG na ERMS). Mapato ya Tume kupitia Mfuko wa Ukaguzi yameongezeka kutoka Shillingi Billioni 2.7 robo ya tatu ya mwaka wa Fedha 2019/20 sawa na ongezeko la asilimia 558.

Kama mnavyofahamu Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS) vimeendelea kuimarisha Uchumi wa wananchi kupitia utoaji wa mikopo kutoka Billioni 889.2 mwaka 2015 hadi kufikia Shillingi Trilioni 1.3 mwaka 2019. Hivyo, tumeendelea kutoa kipaumbele katika uanzishwaji na uendelezwaji wa SACCOS kwa njia mbalimbali ikiwemo kuanzisha mifumo ya TEHAMA ya usimamizi na usajili wa Vyama hivi kupitia mfumo wa Utoaji wa Leseni(SACCOS Licence Online Application System) unaopatikana katika Tovuti ya Tume www.ushirika.go.tz. Nitoe wito kwa Vyama vya Akiba na Mikopo kuendelea kujisajili katika mfumo huu kwa mujibu wa Sheria Na. 10 ya Huduma Ndogo za Fedha (2018) pamoja na Kanuni zake za mwaka 2019.

Tume imeendelea kuimarisha usimamizi wa Sekta ya Ushirika kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu.Katika usimamizi wa Sekta hii Tume imesimamia kufutwa kwa Vyama 3,348 ambavyo vimekuwa havitekelezi wajibu wake kwa mujibu wa Sheria. Hivyo, Rejista ya Vyama vya Ushirika imebaki na Jumla ya Vyama vya Ushirika 8,611. Aidha, Naungana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na mataifa yote Duniani kutoa pole kwa madhara mbalimbali yaliyojitokeza kutokana na ugonjwa wa Covid 19 unaosababishwa na virusi vya Corona. Nitoe wito kwa Wanaushirika na wananchi wote kuendelea kuchukua tahadhari kwa kufuata ushauri na maelekezo ya Wataalamu wa Afya ili kudhibiti maambukizi na kutoa fursa ya kuendelea na shughuli za kiuchumi.

Niwatakie ufuatiliaji mzuri wa habari na makala za Ushirika zilizopo katikaJaridahiliambazo nina tumaini zitaongeza uelewa na maarifa kuhusu utekezaji na mikakati ya Sekta ya Ushirika.

**Karibuni sana!**

# WAKULIMA WATAKIWA KUWA NA VITAMBULISHO- WAZIRI HASUNGA



*Waziri wa Kilimo Mhe. Japhet Hasunga (wa pili kushoto) akioneshwa madaraja ya Tumbaku wakati wa uzinduzi rasmi wa masoko ya minada ya Tumbaku wa mwaka 2020/21 wilaya ya Chunya Mkoani Mbeya*

Waziri wa Kilimo Mhe. Japhet Hasunga ametoa wito kwa wakulima nchini kuwa na Vitambulisho ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa za mkulima kwa urahisi kama vile aina ya kilimo anachofanya, eneo analotoka, mazao anayolima na taarifa nyingine muhimu za utambulisho wake. Aliyasema hayo wakati wa hafla ya uzinduzi rasmi wa masoko ya minada yaTumbaku wa mwaka 2020/21 uliofanyika Wilaya ya Chunya Mkoani Mbeya. Akifungua masoko hayo Waziri alisisitiza kuwa ni muhimu wakulima kuwa na vitambulisho kwani kilimo ni moja ya Sekta muhimu za uchumi wa Taifa letu kutokana na kilimo kuchangia pato la Taifa pamoja na asilimia 30 ya fedha za kigeni kwa mahitaji yakibiashara, ajira, chakula, na malighafi za viwandani.

*"Kila mkulima asajiliwe, ajulikane yuko wapi analima kiasi gani, analima zao gani, analima ukubwa gani wa shamba, kiwango cha mavuno anachopata pamoja na changamoto alizonazo,"* alisisitiza Waziri

Katika hotuba ya ufunguzi huo, Waziri alitoa maelekezo kwa maafisa Ugani wafanye kazi zao kwa bidii wakizingatia kuwahudumia wakulima mashambani. Aliongeza kuwa maafisa ugani watumie muda wao mwingi mashambani ambapo ndipo wanapohitajika kutumia taaluma zao kuongeza uzalishaji wa kilimo chenye tija nchini. Aidha, ameitaka Bodi ya Tumbaku nchini kuongeza kasi ya utafutaji wa masoko ya tumbaku inayozalishwa nchini kutokana na changamoto ya kupungua kwa wanunuzi wa zao la tumbaku pamoja na bei ya zao hilo kuendelea kushuka hivi karibuni. Jambo ambalo linasababisha kipato kwa wakulima kuathirika na mapato ya Serikali kupungua.

Pamoja na mambo mengine ameagiza Viwanda vya tumbaku visiuzwe bali vifufuliwe ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa azma ya Serikali ya kuendeleza na kuimarisha Uchumi wa viwanda, ambapo viwanda hivyo vitatumia mazao na malighafi za kilimo, kuongeza ajira na kukuza Sekta ya Viwanda.

Mrajis waVyama vya Ushirika Dkt. Benson Ndiege akizungumza katika uzinduzi huo amesisitiza Vyama vya Ushirika kuendelea kujikita katika kujenga na kuimarisha mitaji yake ya ndani ili kuwa na nguvu zaidi za kiuchumi katika Vyama itakayowezesha kukopesheka vizuri kwa riba nafuu kutoka kwenye taasisi za Kifedha na mabenki.

Dkt. Ndiege alieleza kuwa Tume ya Maendeleo ya Ushirika kwa kushirikiana na Serikali itaendelea kuchukua hatua dhidi ya wale wote watakaobainika kufanya shughuli za ushirika katika vyama bila kufuata taratibu au watumishi watakaokiuka maadili ya utumishi wa Umma, akimalizia kwa kuwaomba wadau kuendelea kutoa ushirikiano. Kwa upande wake Mwenyekiti wa umoja wa wakulima wa tumbaku Bw. Emmanuel Charahani (T.C.J.E) katika hotuba yake ameelezea baadhi ya changamoto katika kilimo hicho nikuendelea kuporomoka kwa wastani wa bei ya tumbaku. Akifafanua kuwa msimu wa 2016/17 wastani wa bei ulikuwa dola 2.06 lakini msimu huu ambao soko la tumbaku limefunguliwa bei ya wastani ni dola 1.60. Hali inayopelekea wanunuzi na wakulima wa tumbaku kuzidi kupungua na kuiomba Serikali kusaidia kunusuru hali hiyo kwa kutafuta wanunuzi zaidi wa tumbaku.

Charahani amesema matarajio ya kitaifa ni kuzalisha kilo millioni 57 za tumbaku ambazo zinauzwa sasa, hii ikiwa imetokana na hali ya hewa mwaka huu ya mvua nyingi zilizosababisha mbolea kupotea ardhini. Aidha Mwenyekiti Charahani ameipongeza Serikali ya Awamu ya Tano kwa jinsi inavyoendesha na kusimamia shughuli mbambali za kilimo kwa kutetea maslahi ya watu wanyonge. Aliongeza pongezi mahususi kwa Serikali kuondoa baadhi ya tozo na kodi za tumbaku ambazo zitasaidia kujenga hoja zenye nguvu katika kujadiliana bei ya tumbaku.



*Madaraja ya Tumbaku yaliyopangwa tayari kwa mauzo katika ghala lililopo Wilaya ya Chunya Mkoani Mbeya*

# NAIBU WAZIRI BASHE ATAKA USHIRIKA KUJIENDESHA KIBIASHARA



*Naibu Waziri wa Kilimo Mhe. Hussein Bashe akielekeza mikakati ya kuimarisha Ushirika wakati wa kikao cha Makamishna wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika*

Vyama vya Ushirika vimeagizwa kujiendeshe kibiashara kwa kutumia misingi dhabiti ya Ushirika pamoja na matumizi mazuri ya rasilimali zilizopo katika Sekta ya Ushirika ili kutengeneza faida na manufaa kwa Wanaushirika na hatimaye kuongeza pato la Taifa.

Agizo hilo limetolewa na Naibu Waziri wa Kilimo Mhe. Hussein Bashe Mei 7, 2020 wakati wa kikao cha Makamishna wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC) Jijini Dodoma.

Naibu Waziri alieleza Ushirika ni Sekta muhimu kwa uchumi wa Taifa. Hivyo, ikisimamiwa vyema itaweza kutoa mchango mkubwa zaidi kwa wananchi. Alisema Ushirika usiendelee kubaki kama huduma pekee bali uendeshwe kwa kufuata taratibu za kibiashara kama vile kuwa na mifumo dhabiti ya ufuatiliaji wa mauzo, makusanyo ya mazao, malipo pamoja na kuajiri wasomi. Aliongeza kuwa ni lazima Ushirika uongeze thamani ya mazao ili kuuza kwa faida zaidi kuliko kuuza mazao ghafi. *"Ni lazima sasa tufikirie kibiashara zaidi, kwa kusimamia Vyama vya Ushirika vizalishe kwa faida, tuweke mifumo unganishi itakayoweza kuonesha Hii itatusaidia kubaini changamoto na kuzitatua na hatimaye kuondokana na ubadhilifu unaojitokeza mara kwa mara katika Ushirika,"* alisema Bashe

Kufuatia agizo hilo, Naibu Waziri aliitaka Tume ya Maendeleo ya Ushirika kusimamia utekelezaji wa huo kwa kuongeza matumizi ya TEHAMA na kutengeneza mifumo ya kisasa itakayotumika kuwa na taarifa pamoja na kutunza kumbukumbu za Ushirika kuanzia Vyama vya Msingi, Vyama vikuu ili mkulima aweze kupata malipo yake sahihi.

Aidha, Naibu waziri alishauri Ushirika kusajili makampuni ya kibiashara ambayo yatafanya kazi kwa muelekeo wa kibiashara zaidi kwa maslahi ya wanachama. Ushauri huu aliufafanua zaidi kwa kueleza kwamba makampuni ni rahisi kuingia katika makubaliano ya kibiashara, kutambua na kuzitumia fursa mbalimbali za uwekezaji pamoja na utafutaji wa masoko.

Kwa upande wake, Kamishna wa Tume Robert Busumabu alimpongeza Naibu Waziri kwa kuwa miongoni mwa viongozi wa mstari wa mbele katika kusimamia na kufuatilia maendeleo ya Ushirika.Alisema Tume ipo tayari kwa utekelezaji wa maagizo na ushauri muhimu alioutoa na kuahidi kwamba taratibu za utekelezaji zitaanza mara moja kwa kuzingatia misingi ya Ushirika.

# USHIRIKA UJIKITE KATIKA UCHUMI WA VIWANDA- KATIBU MKUU KILIMO



*Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo Bw. Gerald Kusaya akisisitiza jambo wakati wa kikao cha makamishna wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika*

Vyama vya Ushirika vimepewa wito wa kuchakata mazao yanayozalishwa na wakulima kwa kuongeza mnyororo wa thamani kupitia Uchumi wa viwanda ili kuhakikisha mkulima ananufaika zaidi na kilimo pamoja na shughuli za uzalishaji mali.

Hayo yamesemwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo Gerald Kusaya Mei 7, 2020 wakati wa kikao cha Makamishna wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC), Jijini Dodoma.

Katibu Mkuu ameeleza kuwa juhudi za kufufua viwanda vya Ushirika ni muhimu zikafuatiliwa kwa karibu kwa lengo la kuongeza mapato ya Vyama vya Ushirika ili mkulima na jamii inufaike. Aliongeza kuwa kwa kufanya hivyo Ushirika utakuwa ukiunga mkono jitihada za Serikali ya Awamu ya Tano ambayo tayari inaendelea kuweka mazingira wezeshi ya kuanzisha, kuendeleza Viwanda nchini. *"Tutafute mbinu za kuongeza tija katika mazao ya wakulima wetu ili wasiendelee kuuza mazao ghafi, hii itakuwa ni namna bora ya kuimarisha, kurejesha ushirika imara na kuongeza imani ya Wanaushirika,"* alisema Katibu Mkuu.

Akifafanua zaidi suala la viwanda Kusaya alitaja moja ya changamoto zinazowakabili wakulima mara kwa mara wakati wa mavuno ni upatikanaji wa vifungashio hususan magunia. Hivyo, alisema changamoto hizo zigeuzwe kuwa fursa kwa kuagalia namna bora ya uchakataji wa zao la katani kwa lengo la kupata vifungashio kwa urahisi na bei nafuu kwa wakulima. Vilevile, aliongeza kuwa bado mahitaji ya pembejeo hasa mbolea kwa wakulima ni makubwa hali inayoweza kuangaliwa kama fursa nyingine ya uzalishaji wa viwandani hapa nchini, jambo ambalo litampa mkulima nafuu ya gharama za kilimo. Aidha, Katibu Mkuu ameitaka Tume kuendelea kuhamasisha kilimo cha mazao ya kimkakati kama vile Pamba, Tumbaku, Kahawa, Ufuta na Korosho yatakayo ongeza malighafi zinazohitajika kwaajili ya viwanda.Kwa upande wake Kamishna wa Tume Abdul Marombwa alimshukuru Katibu Mkuu kwa maelekezo na ushauri unaoenda kuongeza tija na kasi ya ukuaji wa Sekta ya Ushirika na kuahidi Tume ya Maendeleo ya Ushirika itaendelea kutoa ushirikiano kwa wadau wa Sekta ya Ushirika ili kuhakikisha wanaushirika na Taifa linapata manufaa na viwanda vinaongezeka.

# UJIO WA SHERIA YA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA KULETA SULUHU YA RIBA KUBWA ZA MIKOPO



*Mrajis Msaidizi sehemu ya Usimamizi wa Vyama vya Ushirika wa Vyama vya Kifedha wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Josephat Kisamalala akitoa mada wakati wa mafunzo kwa Viongozi na Watendaji wa Vyama vya Akiba na Mikopo (SACCOS) Jijini Arusha.*

Wananchi wengi hususan wa kipato cha chini wamekuwa ni moja ya kundi ambalo huathirika na huduma zitolewazo na taasisi za huduma ndogo za kifedha kutokana na riba kubwa za mikopo zitolewazo na taasisi hizo, kuwaibia wananchi kwa njia za mitandao mbalimbali,utaratibu mbovu wa ukusanyaji wa madeni uliokuwa ukisababisha wananchi kupoteza mali zao pamoja na changamoto nyingine zilizobainika katika sekta hiyo. Katika kumkomboa mwananchi na changamoto hizo, Serikali ilitunga Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya mwaka 2018 pamoja na Kanuni mahsusi za biashara ya Huduma Ndogo za Fedha za Mwaka 2019 kwa ajili ya kufanikisha utekelezaji wa Sheria husika na kuhamasisha ukuaji na uendelezaji wa Sekta hiyo. Sheria na Kanuni zilitangazwa kuanza kufanya kazi mnamo tarehe 01 Novemba 2019. Benki Kuu ya Tanzania imepewa jukumu la kusimamia taasisi zinazotoa Huduma Ndogo za Fedha nchini kwa kushirikiana na Mamlaka nyingine kama Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC) na Serikali za Mitaa. Ili kufanikisha jukumu hili kwa ufanisi zaidi Benki Kuu ya Tanzania ilikasimisha mamlaka na majukumu yake kwa Tume ya Maendeleo ya Ushirika kupitia Tangazo la Serikali (GN.887).

Tume ambayo kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013 inasimamia Vyama vya Ushirika ikiwemo Vyama vya Akiba na Mikopo (SACCOS).

Naibu Mrajis wa Vyama vya Ushirika Usimamizi na Udhibiti wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Bw. Collins Nyakunga akiongea wakati wa Mafunzo ya Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha kwa Viongozi na Watendaji wa Vyama vya Akiba na Mikopo (SACCOS) Jijini Dar es salaam, alitoa wito kwa Vyama kuwa na uelewa wa Sheria ya Vyama vya Ushirika Na.6 ya mwaka 2013, Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha Na.10 ya mwaka 2018, miongozo na Kanuni husika za Ushirika. *"Viongozi na Watendaji ni lazima kuzijua na kuzifuata Sheria, Kanuni na Taratibu za Ushirika ili kuhakikisha kuwa mnatekeleza majukumu yenu kwa ufanisi na usahihi bila kukinzana na taratibu za Kisheria. Kwa kufanya hivyo, mtavisaidia vyama kuwa endelevu, kujenga na kuongeza imani kwa wanachama,"* alisema Nyakunga

Wakati wa mafunzo hayo Mrajis Msaidizi sehemu ya Usimamizi wa Vyama vya Ushirika wa Vyama vya Kifedha wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Josephat Kisamalala alieleza kuwa watoa huduma ndogo za kifedha wamegawanyika katika madaraja manne Daraja la kwanza ni taasisi zinazopokea Amana, Daraja la pili ni taasisi zisizopokea amana, wakopeshaji binafsi pamoja na watoa huduma kwa njia ya mtandao. Daraja la tatu ni Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS) na Daraja la nne ni Vikundi vya kijamii vya huduma ndogo za fedha kama vile VICOBA. Akieleza masharti ya kanuni za Huduma ndogo za Fedha daraja la tatu hususani Vyama vya Akiba na Mikopo (SACCOS) Kisamalala amefafanua kuwa hivi sasa Vyama hivyo vitakuwa vikifanya kazi kwa kuzingatia masharti maalum yaliyozingatia kulinda maslahi ya wanaushirika.

*"Kutakuwa na makundi mawili ya leseni SACCOS zenye leseni daraja A na daraja B, Kiwango cha chini cha mtaji kwa SACCOS zenye leseni daraja A ni Tsh Milioni 10 na leseni daraja B ni Tsh Milioni 200, SACCOS haitaruhusiwa kutoa huduma ndogo za fedha pasipo kuwa na Leseni ya utoaji wa huduma hizo kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Huduma ndogo za fedha, Iwapo SACCOS itashindwa kufikia kiwango cha chini cha mtaji, SACCOS hiyo itapaswa kuwasilisha mpango wa kuongeza mtaji ndani ya siku 60 tangu ishindwe kufikia mtaji huo kwa Msimamizi,"* amesema Kisamalala

**Shughuli zinazoruhusiwa kufanywa na SACCOS daraja A**

Kwa mujibu wa Sheria ya Huduma ndogo za Fedha Shughuli zinazoruhusiwa kufanyika katika SACCOS daraja A ni pamoja na kupokea hisa za uanachama za hiari, kupokea akiba na kutoa mikopo kwa wanachama, kufanya uwekezaji, kufanya shughuli nyingine zitakazoidhinishwa na Benki Kuu au Mamlaka Kasimishwa.

**Shughuli zinazoruhusiwa kufanywa na SACCOS daraja B**

Shughuli zinazoruhusiwa kufanywa na SACCOS zenye leseni daraja B ni pamoja na shughuli zote zilizoruhusiwa kwa SACCOS zenye leseni daraja A; kupokea amana kutoka kwa wanachama wake, kutoa mikopo shirikishi, kutoa mikopo ya karadha, huduma za uwakala wa bima ndogo, uwakala wa benki, uwekezaji wa mitaji, kutoa kadi za malipo (debit card), kufungua matawi na milango ya huduma na shughuli nyingine zitakazoidhinishwa na Benki Kuu au Mamlaka Kasimishwa.

**Shughuli zisizoruhusiwa kufanywa na SACCOS**

Wanaushirika wanatakiwa kuzingatia Kanuni na Masharti yaliyowekwa ili kuendana na matakwa ya Sheria na taratibu za huduma ndogo za Fedha. Aidha, SACCOS hazitakiwi kuendesha akaunti ya hundi kwa wanachama, kupokea amana kwa wasio wanachama, kufanya biashara ya kubadilisha fedha za kigeni. Vilevile, SACCOS hazitakiwi kufanya shughuli za biashara za nje, shughuli za udhamini, kutoa Credit Cards, kuhamisha fedha na kutoa oda za malipo.

**Utoaji Leseni**

Katika kuboresha utendaji wa Vyama vya Akiba na Mikopo nchini, SACCOS zote zinahitajika kuwa na leseni kwa mujibu wa Sheria ya Huduma ndogo za Fedha. Hivyo, Utaratibu unaelekeza leseni zote zitatolewa na Mrajis wa Vyama vya Ushirika nchini Makao Makuu ya Tume ambapo, Warajis Wasaidizi wa Mikoa na Maafisa Ushirika wa Wilaya watasaidia kutoa maelekezo na kufanya tathmini ya maombi ya leseni zilizoombwa na SACCOS. Maombi yote ya leseni yataombwa kwa njia ya mtandao (SACCOS License online Application System) inayopatikana kwenye tovuti ya Tume www.ushirika.go.tz

*"Leseni zitatolewa na Mrajis wa Vyama vya Ushirika nchini mara baada ya kufanyika kwa tathmini ya maombi hayo kwa kina. Ofisi za Mikoa na Wilaya zitahakikisha zinatoa maelekezo kwenye*

*Vyama na kuhakikisha SACCOS zote zilizopo katika maeneo yao zinatekeleza matakwa ya Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha"*, alisema Kisamalala Mfumo wa utoaji leseni unaenda kuongeza ufanisi kwa kusaidia upatikanaji wa ripoti za Vyama

vilivyoomba leseni, zilizopata leseni, kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa wanaushirika popote walipo kupitia mifumo ya TEHAMA. Hivyo wanaushirika kupata huduma kwa haraka bila kulazimika kusafiri kutoka eneolake. Kwa upande wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika mfumo huu utasaidia kuboresha taarifa za waombaji leseni wakati wowote zinapohitajika kutokana na kanzidata zenye taarifa sahihi.

Aidha, Kisamalala alieleza kuwa ili kuimarisha na kuwajengea uwezo Viongozi na Watendaji wa Vyama vya Akiba na Mikopo nchini hususan katika kutimiza wajibu wao kwa mujibu wa Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha, Tume tayari imeshafanya mafunzo kwa Viongozi na Watendaji katika kwa jumla ya SACCOS 755 zikiwa na viongozi na watendaji 1,350 na Maafisa 119. Mafunzo hayo yamefanyika katika mikoa mbalimbali ikiwemo Kagera, Mwanza, Mbeya, Singida, Korogwe, Songwe, Shinyanga, Ruvuma, Kilimanjaro, Dar es salaam, Pwani, Iringa na Arusha.

Mrajis huyo alifafanua kuwa mafunzo hayo yatakuwa ni endelevu kulingana na mahitaji ya wadau, akiongeza kuwa Tume inaendelea na utoaji elimu kwa njia mbalimbali hususani matumizi ya Vyombo vya habari ili kufikisha elimu hiyo kwa wadau wengi zaidi.

Mtendaji Mkuu wa Chama Kikuu cha Akiba na Mikopo (SCCULT), Hassan Mnyone akiwasilisha mada wakati wa mafunzo yaliyoandaliwa na Tume kuhusu Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha kwa Viongozi na Watendaji wa Vyama vya Akiba na Mikopo Jijini Arusha, amepongeza kutungwa Sheria hiyo kwa kuwa inaenda kuongeza tija katika Vyama vya Kifedha kutokana na malengo ya kuwalinda watumiaji wa huduma za fedha kama vile kutoa riba na gawio, kutoa taarifa na takwimu zinazohusu uendeshaji wa taasisi kwa wakati pamoja na kuwekautaratibu wa ukusanyaji wa madeni.



*Viongozi na Watendaji wa Vyama vya Akiba na Mikopo (SACCOS) wakifuatilia mada za mafunzo ya Sheria Na.10 ya Huduma Ndogo za Fedha yaliyokuwa yakiendeshwa na Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Jijini Dar es salaam*

# USHIRIKA UNAVYOWAKOMBOA WANAWAKE



*Wanawake wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika wakiwa na vifaa mbalimbali tayari kwa kuwasilisha kwa Wanawake wahitaji, Jijini Dodoma ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani*

Utakuwa umewahi kusikia maneno yasemayo kuwa ukimuelimisha mwanamke umeielimisha Jamii, sambamba na hilo mwanamke akiimarika kiuchumi jamii imeimarika, kwa kuwa familia inapata uhakika wa maisha bora kadhalika Jamii na Taifa kwa ujumla. Vyama vya Ushirika nchini vimekuwa ni chachu ya maendeleo na ukombozi wa wanawake kupitia fursa mbalimbali zilizomo katika Vyama hivyo ikiwemo Kilimo, ufugaji, uvuvi, madini pamoja na vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS). Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) inayoundwa na Sheria Na.6 ya Vyama vya Ushirika ya mwaka 2013 inasimamia Vyama hivyo katika kuhakikisha kuwa vinajiendesha kwa kufuata Sheria, Kanuni na Taratibu kwa uendelevu na maslahi ya wananchi.

Consolata Kiluma, Mwenyekiti wa Wanawake katika Tume ya Maendeleo ya Ushirika wakati wa mahojiano maalum ya makala hii wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani ametoa wito kwa wananwake kuchangamkia fursa zilizopo katika Sekta ya Ushirika ili kujikwamua kiuchumi na kuleta maendeleo katika Jamii zao. Alieleza kuwa Ushiriki wa Wanawake katika Ushirika bado ni mdogo na kuongeza kuwa wanawake wengi wanaweza kuzitumia fursa za kiuchumi kupitia Vyama vya ushirika hususan vyama vya Akiba na Mikopo (SACCOS) kutokana na riba nafuu zinazotolewa na Vyama hivyo katika maeneo mengi mijini na vijijini, vyama vya mazao (AMCOS) pamoja na viwanda vitokanavyo na shughuli za Ushirika.

Kiluma alisisitiza wanawake wasiache fursa za Ushirika zikawapita au zikatumika na wanaume peke yake badala yake wawe mstari wa mbele kujua fursa hizo na kuzitumia ipasavyo. Akionesha kuwa kwa kufanya hivyo wanawake watakuwa wakienda sambamba na iliyokuwa Kauli mbiu ya mwaka huu 2020 isemayo "Kizazi cha usawa kwa Maendeleo ya Tanzania ya sasa na baadaye"

Akizungumzia manufaa ya Ushirika kwa Wanawake, Mwenyekiti wa Chama cha Ushirika cha Wanawake cha kukusanya na kusindika maziwa cha Nronga Women Diary CooperativeSociety Hellen Usiri kilichopo Wilayani Hai mkoa wa Kilimanjaro alieleza kuwa Chama hicho kimekuwa kikiendesha shughuli zake hadi kuanzisha Kiwanda cha Usindikaji wa maziwa ambacho kinauza bidhaa kwa ubunifu mkubwa hadi kuwa na ATM ya maziwa, ambapo mteja analipa fedha na kupata maziwa kwa mashine ya ATM. Jambo ambalo limepongezwa na Mwenyekiti wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Dkt. Titus Kamani katika ziara ya kujionea shughuli za kiwanda hicho kinachomilikiwa na wanawake wa Ushirika wa Nronga na kusema kuwa Ushirika huo utaendelea kuongeza wigo wa fursa za uchumi, ajira na hasa azma ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kuifanya Tanzania nchi ya Uchumi wa Kati kupitia "Uchumi wa Viwanda" *"Nimeona ari ya kinamama inavyoweza kubadilisha uchumi wa eneo, licha ya kutengeneza fedha pia kuongeza ajira kwa kukusanya, kusindika na kuuza bidhaa za maziwa zenye ubora na kupata masoko katika maeneo mbalimbali kwa urahisi kupitia Ushirika,"* alisema Dkt. Kamani

Nae Mwenyekiti wa Chama cha Ushirika cha Akiba na Mikopo cha Wanawake wa Wilaya ya Karagwe na Kyerwa kilichopo Mkoani Kagera kiitwacho Kagera Women Saving and Credit Cooperative Society Ltd (KAWOSA) Safina Amrani amesema chama hicho kilianza na wanachama waanzilishi wanawake 70 mwaka 2006 kimekuwa na kufikia jumla ya wanachama 11,643. Akiongeza kuwa KAWOSA ilianza na mtaji wa kiasi cha Shillingi 1,000,000/- na mpaka sasa mtaji huo umekuwa hadi kufikia kiasi cha Shillingi 1,500,000,000/-. Akibainisha kuwa ukuaji wa mtaji wa Chama ni matokeo ya wanachama ambao ni kinamama kuwa na bidii ya kazi na uaminifu, ambapo wanachama hao hukopa fedha kwa ajili ya miradi mbalimbali pamoja na kilimo na kizirejesha kwa kuzingatia masharti waliyowekeana. "KAWOSA ni chama kilichoanza na changamoto nyingi zikiwemo kutokuwa na miundombinu ya utendaji kama vile majengo ya ofisi na vitendea kazi, kwakweli hatukukata tamaa tuliendelea kuhamasishana na hata ilipobidi wanachama walikutana chini ya mti kila tarehe 5 ya mwezi na kuendelea kujadili na kutekeleza majukumu yetu. Hivyo, natoa wito wanawake tusikate tamaa katika harakati za kujikwamua kiuchumi licha ya changamoto zinazoweza kuwepo hasa katika hatua za awali," alisema Safina

Meneja wa Chama cha KAWOSA Goreth Elias amesema chama hicho kimekuwa kikizingatia matakwa ya Sheria, Kanuni na taratibu za Vyama vya Ushirika. Chama hicho licha ya kutoa mikopo kwa mwanachama mmoja mmoja vilevile wana utaratibu wa kutoa mikopo kwa vikundi vya wanawake wa kipato cha chini ili kuwawezesha kujikwamua




*Wanawake wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika wakiwa katika maandamano ya maadhimisho ya Siku ya Wanawake yaliyofanyika Kata ya Mkonze, Mkoani Dodoma*

# WAKULIMA WAHAMASISHWA KUWEKA AKIBA



*Mrajis wa Vyama vya Ushirika Dkt. Benson Ndiege (wa pili kulia) akipata maelezo ya Shamba la Skimu ya Umwagiliaji ya Chama cha Ushirika cha Wakulima Wadogo wadogo wa Mpunga Dakawa (UWAWAKUDA) kutoka kwa Mwenyekiti wa Chama hicho Bw. Thomas Kalema, alipokuwa kwenye ziara ya kikazi Mkoani Morogoro*

Wakulima wa Vyama vya Ushirika nchini wamepewa wito wa kuboresha maisha yao kwa kuweka akiba baada ya msimu wa mavuno ya mazao yao ili akiba hizo ziwasaidie hususan wanapopata changamoto mbalimbali za kimaisha. Wito huo umetolewa na Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC) Dkt. Benson Ndiege wakati alipotembelea Chama cha Ushirika wa Wakulima wadogo wadogo wa Kilimo cha umwagiliaji Mpunga Dakawa (UWAWAKUDA LTD) kwenye ziara ya Kikazi, Mkoani Morogoro.

Mrajis alisema kuwa wanachama wa Ushirika wanaweza kutumia fursa ya kuwa pamoja katika Chama kwa kuimarisha Ushirika wao kwa kujiwekea utaratibu maalum wa kutunza akiba zinazotokana na mauzo ya mazao pale wanapovuna. Alibainisha kuwa utaratibu huo utakaposimamiwa vizuri kwa taratibu za kiushirika unaweza kuongeza fursa nyingine ya kuwa na Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS) inayotokana na wanachama wa UWAWAKUDA.

*"Kila mkulima anapovuna anaweza kujiwekea Akiba katika Mfuko wao ambao utatumiwa na Wanaushirika kwa mahitaji yao mbalimbali pamoja na dharura zinapojitokeza kwa mwanachama,"* alisema Mrajis

Aidha, Akielezea Chama hicho Mwenyekiti wa UWAWAKUDA Bw. Thomas Kalema alisema kuwa Chama hicho cha Ushirika chenye jumla ya Eka 5,000 za umwagiliaji kilianzishwa rasmi tarehe 24 Julai 2006 kina Jumla ya Wanachama 935 ambao kati ya hao 552 ni wanaume, 376 ni wanawake pamoja taasisi za kidini 7. Alibainisha kuwa Mradi huo umekuwa ukipata ufadhili kutoka Serikalini pamoja na wadau wengine wa maendeleo kwa lengo la kuwakomboa wananchi kiuchumi.

Makamu Mwenyekiti wa Chama hicho Bertha Chilosa alipata fursa ya kueleza kuwa kabla ya kuanzishwa kwa Ushirika miaka ya 2004 kurudi nyuma, hali ya maisha ya wakazi wa Dakawa ilikuwa duni sana ukilinanisha na baada ya Ushirika kuanzishwa.

Alibainisha baadhi ya manufaa yaliyopatikana na mradi huo ni pamoja na Wanachama wengi kuweza kujenga nyumba bora za kisasa, fursa za mikopo kwenye taasisi za kifedha, huduma kwa jamii, upatikanaji wa ajira akitoa mfano kuwa zaidi ya vibarua 5,000 kutoka Dakawa na maeneo jirani katika kipindi cha msimu wa kilimo. Aliongeza kuwa vijana wengi kupitia shamba la UWAWAKUDA wamefungua biashara mbalimbali zinazowasaidia kuhudumia familia na kuchangia pato la Taifa.



*Mrajis wa Vyama vya Ushirika Dkt. Benson Ndiege akioneshwa mitambo ya Pampu za maji za mradi wa Skimu ya Umwagiliaji wa UWAWAKUDA, Dakawa Mkoani Morogoro*

# CHAMA CHA USHIRIKA WA MAZIWA AYALABE-KARATU USHIRIKA UNAVYOTEKELEZA AJENDA YA VIWANDA KWA VITENDO



*Mtaalamu wa Kitengo cha Vifungashio Hadija Mandi wa Kiwanda cha Ushirika wa Maziwa cha Ayalabe Diary akielezea kuhusu Karatu Milk walipotembelea Kiwanda hicho kilichopo Wilaya ya Karatu, mkoani Arusha*

"*Hatuna njia nyingine kama kweli tunataka kujenga msingi wa uchumi endelevu katika nchi yetu, na maisha ya watu wetu. Dira ya Maendeleo ya 2025 inatutaka tuwe nchi ya watu wenye kipato cha kati."* Hii ni kauli ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,

Mheshimiwa John Pombe Magufuli,akihutubia Bunge la 11 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Novemba 20, 2015 Jijini Dodoma.Serikali ya Awamu ya Tano imekuwa mstari wa mbele katika kuinua uchumi wa nchi kwa azma ya kuifikisha Tanzania katika uchumi wa kati kupitia kipaumbele cha uchumi wa viwanda.

Mrajis wa Vyama vya Ushirika nchini na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika nchini (TCDC), Dkt. Benson Ndiege katika mahojiano ya Makala hii ameeleza kuwa Ushirika ni miongoni mwa Sekta muhimu zenye mchango kiuchumi hususan katika kuendeleza na kukuza viwanda nchini.

Mrajis alibainisha kuwa Ushirika ni Sekta pana yenye uwezo wa kutoa mchango kupitia nyanja mbalimbali kama vile kilimo, ufugaji na madini kupitia hitaji muhimu la uendeshaji wa viwanda hususan uzalishaji wa malighafi zinazohitajika viwandani pamoja na uchakataji wa malighafi hizo ili kuongeza mnyororo wa thamani wa mazao ya wanaushirika.

Dkt. Ndiege aliongeza kuwa Ushirika unaweza kutumika kama nyenzo muhimu ya kuwaunganisha wakulima, wafugaji, wachimbaji kupitia nguvu ya pamoja kuzalisha kiwango kikubwa cha malighafi za viwanda kuliko uzalishaji wa mtu mmoja mmoja.

Mrajis alifafanua kuwa vyama hivi vinaweza kutumika kuzalisha malighafi za viwandani,

kuanzisha viwanda vya uchakataji wa malighafi, kuongeza thamani ya mazao, kuchangia mitaji ya kuanzisha viwanda au kuwa na miradi ya pamoja yenye malengo ya uzalishaji wa bidhaa za viwandani. *"Ushirika nchini unaenda sambamba na muelekeo wa Serikali ya Awamu ya Tano wa kuimarisha na kuifikia Tanzania ya Viwanda, kwani vyama vina rasilimali watu, fedha, na malighafi zinazoweza kutumika kufikia Uchumi wa Viwanda na faida itakayopatikana itarudi kwa wanaushirika na Taifa kunufaika,"* alisema Dkt. Ndiege.

**Kiwanda cha Usindikaji Maziwa cha Ayalabe Diary**

Bwana Godlisten Mayyo, Mwenyekiti wa Chama cha Ushirika wa Maziwa kinachomiliki Kiwanda cha usindikaji maziwa cha Ayalabe Diary kinachozalisha maziwa ya Karatu Milk kilichopo Wilaya ya Karatu Mkoani Arusha anasema Kiwanda hicho kimeanza uzalishaji Machi 2020 baada ya kusitisha uzalishaji kutokana na changamoto zilizokuwepo awali. Akielezea Historia Chama hicho Mayyo alisema Chama hicho kilianza na wanachama 40 hadi hivi sasa wana jumla ya wanachama 240 ambao waliungana kwa pamoja na kuanzisha Kiwanda cha kusindika maziwa kutokana na wengi wao kuwa wafugaji wa ng'ombe. Mwenyekiti alieleza kuwa Kiwanda hicho kimekuwa ni soko zuri kwa wafugaji wanachama na hata wakazi wa eneo la Karatu na maeneo mengine jirani. Maziwa ya Karatu Milk huuzwa Karatu, Arusha na maeneo mengine, na kiwanda kina mikakati ya mbeleni ya kuangalia namna bora ya kuongeza soko la bidhaa hiyo.

**Uzalishaji wa Maziwa**

Meneja Uzalishaji wa Kiwanda hicho, Omari Cuba alibainisha kuwa katika kuhakikisha kuwa Kiwanda hicho kinazalisha bidhaa kwa kuzingatia ubora. Alifafanua kuwa maziwa yanapopokelewa kiwandani hufanyiwa vipimo vya aina tofauti kama vile kuchunguza kitaalamu kiwango cha maji, joto, uzito na masuala mengine yahusuyo ubora wa maziwa.

Cuba alieleza vipimo hivyo hufanyika kudhibiti malighafi hiyo iweze kuchakatwa na kupatikana maziwa safi, bora na salama kwa watumiaji. Baadhi ya bidhaa za maziwa zinazozalishwa kiwandani hapo zilitajwa kuwa ni pamoja na cheese, yoghurt za aina tofauti, mtindi, samli na butter. Mtaalamu huyo alielezwa kuwa kwa sasa kiwanda kina uwezo wa kusindika kiasi cha lita 5,000 kwa siku kiwango ambacho kinatarajia kuongezeka kulingana na mahitaji ya bidhaa hiyo ya maziwa kwa kuwa ni maziwa yanayotumika kwa matumizi mbalimbali binafsi pamoja na biashara Wilayani Karatu.

**Mafunzo kwa Wanachama**

Wafugaji wanaopeleka maziwa kiwandani hapo hupata fursa ya mafunzo kuhusu namna bora ya kuzalisha maziwa yanayofaa kwaajili ya usindikaji wa maziwa. Hatua hii hufanyika mara kwa mara ikiwa ni sehemu ya kuhakikisha kuwa wafugaji wanakuwa na uwelewa sahihi wa utunzaji wa maziwa na uzalishaji unakuwa endelevu kwaajili ya kiwanda.

Katika hatua nyingine, Tume ya Maendeleo ya Ushirika katika kuwajengea uwezo viongozi na wajumbe wa Bodi ya Chama hicho iliendesha mafunzo elekezi kwa Wajumbe wa Bodi wa Ayalabe yaliyofanyika hivi karibuni. Mafunzo yaliyofunguliwa na Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika mkoani Arusha Emmanuel Sanka ambaye alichukua fursa hiyo kuwasisitiza Wajumbe wa Bodi kusimamia Kiwanda cha Chama hicho kwa kuzingatia misingi ya Ushirika. *"Wajumbe wa Bodi mnao wajibu wa kusimamia Kiwanda hiki kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Ushirika. Niwaombe kuweka uzalendo na uadilifu mbele kwa maslahi ya Wanaushirika na Taifa kwa Ujumla.Mimi na Ofisi yangu tutakuwa bega kwa bega nanyi katika shughuli zozote zinazohitaji ushirikiano wa pamoja ili kuhakikisha Kiwanda kinaimarika na bidhaa zetu zinapata soko pana zaidi,"* alisema Sanka

Kwa upande wake Mfanyabiashara wa Karatu mjini Cecilia Lawrence ambaye anauza maziwa ya Karatu Milk anasema maziwa hayo ni mazuri, wateja wanayapenda na wanayafurahia. Cecilia alibainisha kuwa uzalishaji wa Kiwanda cha Ayalabe ni faida kubwa kwa wafanyabiashara kwa kuwa imewapa urahisi wa usafirishaji wa bidhaa hiyo ambayo awali walikuwa wakipata kutoka maeneo mengine ya mbali hali iliyosababisha bidhaa hiyo kuuzwa kwa bei ya juu kuliko ilivyo hivi sasa.




*Meneja Uzalishaji wa Kiwanda Omary Cuba akiwa katika shughuli za Usindikaji na utengenezaji wa bidhaa za maziwa katika Kiwanda cha Ayalabe, Karatu Mkoani Arusha*

TCDC
Together We Build
Our Economy

# JE, WAJUA WATOA HUDUMA WANAVYOONGEZA KASI YA MAENDELEO YA USHIRIKA?



*Katibu wa Watoa Huduma Leah Mbilinyi akisoma taarifa ya utendaji kwa watoa huduma wakati wa kikao kazi cha Watoa Huduma kilichoratibiwa na Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Jijini Dodoma*

Vyama vya ushirika nchini vimekuwa ni vyombo Madhubuti na muhimili wa kuunganisha na kujenga uchumi imara wa wananchi wake kwa pamoja na kuleta ushirikiano wa hali ya juu kwenye jamii.

Kama tunavyofahamu vyama hivi vinaanzishwa kwa hiari ya wanachama kwa kufuata sheria za ushirika na vile vinavyotumia mifumo ya kifedha kwa kutumia sheria ya huduma ndogo za kifedha lakini vinasimamiwa na kudhibitiwa na Tume ya maendeleo ya Ushirika nchini (TCDC) lengo ni kufanikisha ukuaji wa wanachama wake kwa demokrasia na usawa.

Kwa muda mrefu nchini kumekuwa na wadau mbalimbali wanaofanya kazi na vyama vya ushirika kwa madhumuni mazuri tu ya kufanikisha ufanisi wake na kama sehemu ya kukuza vipato kwa taasisi zao. Soko hili likawa huria na kutokufikiwa viwango mahususi na kutotambulika na mthibiti na msimamizi mkuu wa vyama hivi hata kufikia baadhi ya vyama kutofanya vyema kwa kutofuata sheria na utaratibu husiika.

Mwaka 2016, Tume ya maendeleo ya ushirika nchini kupitia kitengo chake cha Utafiti na mafunzo, ikaona vyema kuanzisha uwepo wa watoa huduma ili kushirikiana nao na kuwapatia elimu husika ya ushirika sambamba na kuendana na taratibu , sheria na sera kuweza kufanikishga ufanisi na ukuaji wa vyama vya ushirika na kuwa na takwimu sahihi kwa wakati katika utendaji kazi.

Serikali kupitia Tume ya maendeleo ua Ushirika nchini katika utekelezaji wa sera ya uchuni na soko huru na ubinafsishaji ya mwaka 2002 na sheria ya ushirika nchini Na. 6 ya mwaka 2013 kimkakati, ilitutambua watoa huduma na kuanza kufanya kazi kama wabia kwa kuhusisha taasisi mbalimbali kwa lengo la kuongeza ushindani na tija kwa vyama na wanachama.

Kitengo cha utafiti na mafunzo kiligundua changamoto kubwa ni kwamba, kulingana na mfumo wa uchumi, vyama vya ushirika nchini vinapata ugumu wa kupata huduma na mitaji, kutofanyika kwa ukaguzi kwa wakati husika, mifumo ya kiukaguzi na mahesabu isiyoeleweka na kukidhi mahitaji ya chama, walanguzi wa mazao ya wakulima, uhaba na uhafifu wa mafunzo kwa wanachama, madeni sugu yasiyoweza kurudishwa na kusababishia hasara kubwa sana ya vyama. Hivyo basi, watoa huduma wakaonekana wana umuhimu sana ili kuweza kubeba hizo changamoto na kuziweka katika hali rafiki ya kuweza kukuza uchumi wa vyama vya ushirika. Serikali ikaandaa muongozo ambao utasaidia watoa huduma kuto kukiuka utaratibu katika utoaji huduma na sambamba kuendana na sharia ambazo ni mahususi kabisa katika vyama vyetu na kuleta tija. Kuanzia mwaka 2016/2017 mpaka kufikia mwaka 2019/2020 Tume ya maendeleo ya ushirika imeweza kutoa vibali ambavyo vinatiumika kama muongozo wa kufanya kazi kwenye vyama vya ushirika kwa kufuatilia utoaji kazi n ahata hivyo kuwa na mamlaka ya kufuta vibali ambavyo wadau hawajawa na weledi katika kufanya kazi na kukosa uaminifu.

## Mtoa Huduma ni nani?

Mtoa huduma ni taasisi binafsi, au taasisi ya kiserikali/ zisizo za kiserikali zenye ujuzi Fulani/ maalumu ambazo zina uwezo wa kusaidia vyama vya ushirika bila kuvunja maadili wala sheria ya ushirika sambamba na kuendana na misingi ya ushirika.

Kwa mwaka 2020/2021 watoa huduma wote kwenye vyama vya ushirika wanahitajika kuwa na elimu ya ushirika itakayosimamiwa na kutolewa na chuo kikuu cha ushirika Moshi. Lengo ni kuhakikisha huduma zitolewazo hazina vikwazo kwa vyama vya ushirika.

## Huduma zipi zinatolewa na watoa huduma kwenye vyama vya ushirika?

Kutokana na malengo ya Tume ya maendeleo ya Ushirika kwa kushirikiana na vyama vya ushirika nchini, ikaona ni vyema kuwa na wadau mbalimbali katika kushirikiana hivyo kuweka huduma zifuatazo kuwa ndo muhimili utakaojengwa na watoa huduma.

1. Huduma za TEHAMA (Teknolojia ya habari na mawasiliano)
2. Huduma ya ukusanyaji madeni sugu
3. Huduma ya kujengea uwezo vyama vya ushirika na ushauri wa kitaalamu
4. Huduma za kuandaa takwimu
5. Huduma za bima (Kinga zidi ya majanga) na benki
6. Huduma za ukaguzi wa mahesabu katika vyama vya ushirika

Huduma zote tajwa zinafanywa kwa kibali maalumu na muda maalumu, na wanachama wana haki kutoa taarifa kwenye uongozi wa watoa huduma juu ya hali tete yoyote itakayoleta sintofahamu katika vyama, na uongozi husika utawasilisha Tume ya maendeleo husika na kuchukua hatua stahiki.

Watoa huduma wote walioidhinishwa naTume ya maendeleo ya ushirika sambamba na mawasiliano yao yapo katika tovuti ya tume unaweza kuingia https://www.ushirika.go.tz/services-providers

## Mafanikio Kutokana Na Watoa Huduma Kwenye Vyama Vya Ushirika

➤Kuleta mapinduzi ya kiteknolojia kwenye vyama vya ushirika na kusababisha kuendana na mabadiliko ya sheria

➤Kukusanya madeni yaliyoshindikana kwa muda mrefu hivyo kurejesha Imani ya wanachama kwenye vyama vyao na kuongeza mitaji

➤Kuendelea kupata takwimu husika ambazo zinasaidia serikali katika kutoa tathimini yenye uhalisia kwa wakati

- Kuimarisha mitaji ya vyama vya ushirika kwa kupata elimu ya kuinua vyama katika uwekezaji wake
- Kujengea uwezo vyama katika kulinda biashara zao na kuendana na ushindani
- Kukinga mali za vyama dhidi ya majanga na kuboresha vyama
- Kuandaliwa vitabu vya uhasibu kwa wakati na kusababisha ukaguzi kuwa sio swala lenye changamoto
- Kujenga ushirikiano mzuri na wadau mbalimbali katika kujenga ushirika imara, wenye nguvu na endelevu

Uwepo wa wadau hawa muhimu kumeongeza chachu ya ushindani hivyo kuwa kama kichocheo cha ukuaji wa vyama vya ushirika na kuziweza taasisi hizi katika muhimili imara. Kutokana na ukuaji wa kiuchumi ubia wa serikari na taasisi binafsi ndio umekuwa kiungo kikuu cha kuimarisha usimamizi katika taasisi zinazosimamiwa.

Katika kuboresha ushirikiano huu, maafisa ushirika, wadau wa ushirika(SCCULT, NOSACCU, TFC na MOCu), warajisi wasaidizi tunashirikiana nao bega kwa bega ili kuimarisha shughuli za ushirika kusonga mbele na kuwa mfano bora katika bara letu la Afrika



*Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika (tatu kushoto) Dkt. Benson Ndiege akiwa amekaa kwenye picha ya pamoja na Watoa Huduma mbalimbali wa Vyama vya Ushirikapamoja na Watumishi wa Tume baada ya kikao kazi kilichofanyika, Jijini Dodoma*

Our Economy

# DONDOO ZA USHIRIKA



**JE, NI VYAMA VIPI VYA USHIRIKA VINAVYOHUSIKA NA UCHAGUZI?**

Vyama vinavyohusika katika Uchaguzi wa Viongozi ni Vyama vyote vya Ushirika ambavyo Kalenda za Uchaguzi wa Vyama hivyo zinaonyesha kuwa wanatakiwa kufanya uchaguzi kwa wakati husika. Vyama hivyo ni pamoja na Vyama vya Ushirika vya Msingi, Vyama Vikuu, Miradi ya pamoja ya Ushirika, ubia wa Vyama vya Ushirika na Shirikisho kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Masharti ya Ushirika uchaguzi wa Viongozi hufanyika kila baada ya miaka mitatu ambapo viongozi waliopo madarakani wanakuwa wamemaliza kipindi chao cha uongozi.

# IJUE SCCULT (1992) LTD



*Mwenyekiti wa SCCULT Dkt. Gervas Machimu akitoa mada kwa wajumbe wa Mkutano Mkuu wa 22 wa Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Ushirika wa Akiba na Mikopo Kitaifa (ICUD) uliofanyika Mkoani Arusha*

SCCULT (1992) LTD ni Chama Kikuu cha Ushirika wa Akiba na Mikopo ambacho kinaundwa na Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo Tanzania Bara. Chama hiki kilianzishwa tarehe 19/10/1992 chini ya Sheria ya Ushirika namba 15 ya Mwaka 1991 kikiwa na malengo ya kufanya shughuli mbalimbali zitakazosaidia Uboreshaji wa utendaji kazi wa Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo Nchini

Dhamira ya SCCULT (1992) LTD imekuwa ni kuona SACCOS zinatoa huduma bora kwa wanachama wake na SACCOS zenyewe zinaendelea kuwa taasisi imara wakati wote.

**I. Nani Anaweza Kuwa Mwanachama Wa Sccult (1992) Ltd?**

Ni Chama chochote cha Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS) ambacho kimesajiliwa na kuandikishwa na Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC)

**II. Kuna Umuhimu Gani Wa Kuwa Mwana-chama Wa Sccult (1992) Ltd?**

a) Kuwa kwenye Umoja wa Vyama wa SACCOS Tanzania kwa ajili ya Utetezi, Uwakilishi na Uzengezi.
b) Kuwa na uwezo wa kuingia makubaliano ya pamoja na maamuzi ya pamoja juu ya mambo mbalimbali kama kupambana dhidi ya Sera, Sheria, matamko mbalimbali kandamizi dhidi ya sekta ya Ushirika wa Akiba na Mikopo.
c) Kuwa na chombo imara kwa ustawi na ukuwaji wa SACCOS Tanzania chenye maslahi chanya na sekta na kinachomilikiwa na wana SACCOS wenyewe.

## III. Nini Kazi Za Sccult (1992) Ltd?

a. Ujenzi wa uwezo kwa SACCOS na wadau wake kwa kuendesha Mafunzo mbalimbali ambayo yanasaidia kuwajenga wanachama, wajumbe wa Bodi na watendaji na wadau wa sekta.

b. Utetezi, Uwakilishi na Uzengezi SCCULT (1992) Ltd inafanya kazi ya kutetea vyama wanachama dhidi ya mambo yanayo kandamiza na kudumaza sekta. Kuwakilisha SACCOS katika hatua mbalimbali ndani na nje ya nchi. Kufanya uzengezi wa kuzitafutia fursa mbalimbali ambazo zenye maslahi na kuijenga sekta hii nyeti ya kifedha.

c.Kutoa huduma za kitaalum kwa SACCOS kama ushauri wa kisheria, kihasibu, utengenezaji wa sera mpango kazi mpango mkakati na ushauru mbalimbali wa Uendeshaji wa SACCOS.

d. Uuzaji wa shajala zakiuhasibu na huduma ya kitehama kwa SACCOS.

## Maboresho Ya Sccult (1992) Ltd

SCCULT (1992) LTD inajivunia mambo mengi sana kwa kipindi hiki, mambo hayo ni pamoja na:

1. Kuendelea kuboresha mahusiano yake na wadau muhimu kisekta kama TCDC, COASCO, MoCU, TFC

2. Kuwa na mahusiano mazuri na Serikali kupitia Wizara mbalimbali kama Wizara ya Kilimo, Wizara ya Fedha na Mipango, Benki Kuu ya Tanzania

3. SCCULT (1992) LTD ni mwanachama hai wa Shirikisho la Ushirika wa Akiba na Mikopo Afrika (ACCOSCA)na imeendelea kufungua milango kwenye ushiriki wa watanzania kwenye Mikutano na Makongamano ya Kitaifa kwenye Nchi mbalimbali Duniani ambayo yamekuwa chachu ya mabadiliko chanya kwa kusaidia kubadilishana uzoefu na stadi mbalimbali na wadau kutoa Nchi nyingine Duniani

4. Kusimamia vyema maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Ushirika wa Akiba na Mikopo Duniani (ICUD) kwa kushirikiana vizuri na Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania

5. Kuwa sehemu ya Maandalizi ya Sera na Miongozo kwaajili ya utekelezaji wa Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya mwaka 2018 na Kanuni zake za Mwaka 2019

6. SCCULT (1992) LTD inajipanga kufanya mapinduzi kwenye Masuala ya TEHAMA na Teknolojia kwa SACCOS kuanzia mwishoni mwa mwaka 2020

7. Kuendeleza mahusiano na wadau muhimu na wahisani kwaajili ya utekelezaji wa miradi yenye tija kwa SACCOS

8. Kuendelea kusimamia ufuataji wa Sheria na taratibu za Sekta ya Ushirika na Huduma Ndogo za kifedha ili kuwa na Sekta salama yenye mwamko na watu makini





*Pichani ni wanachama wa SCCULT (1992) LTD wakiwa kwenye mkutano mkuu wa 22, Jijini Arusha*



*Gari aina ya Toyota Hilux lililonunuliwa na Chama Kikuu kwa kushirikiana na Vyama vya Ushirika wanachama wa LATCU linalosaidia Ofisi ya Mrajis Msaidizi (M) - Katavi kufanya majukumu ya ushirika.*

# KATAVI ILIVYODHAMIRIA KUKUZA UCHUMI KUPITIA USHIRIKA



*Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Mhe. Juma Homera akiwa pamoja na Mraji Msaidizi Mkoa wa Katavi, Kakozi Amri wakingea na Wanahabari (hawapo pichani)*

Ushirika ni Moyo wa Uchumi wa Mwananchi mmoja mmoja katika ngazi mbalimbali kwenye ngazi ya Kijiji, Kata, Tarafa, Wilaya, Mkoa hadi Taifa. Katika mkoa wa Katavi, vyama vya ushirika vya aina mbalimbali vimeanzishwa vikiwemo vya wakulima wa mazao mchanganyiko, wafugaji, wavuvi na vyama vya Akiba na Mikopo (SACCOS).

Katika kumkokomboa mkulima, mkoa wa Katavi umeanzisha na kusimamia ipasavyo Mfumo wa Stakabadhi za Ghala ili kumpatia bei nzuri na kuondoa mnyororo wa mtu wa kati aliyekuwa akinunua mazao ya wakulima kwa bei ya chini na kujipatia faida kubwa. Mfumo huu umekuwa ukitekelezwa kupitia masoko ya wazi na soko la bidhaa (TMX).

Akizungumza katika mahojiano maalum Mjini Mpanda, Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Mhe. Juma Homera, amesema kuwa mkoa wa Katavi umedhamiria kuimarisha masoko ya mazao ya wakulima ili yaweze kuwapatia bei nzuri na kuwezesha kuinua maisha ya mkulima mmoja mmoja na uchumi wa mkoa kwa ujumla.

*"Katika kuimarisha kilimo na masoko bora, kwa ajili ya kumkomboa mkulima wa mkoa wa Katavi tumeanzisha Stakabadhi ya Mazao Ghalani ambayo inaendelea kufanya vizuri sana katika mkoa wetu wa Katavi kwa lengo la kukatamnyororo wa mtu wa kati ambaye anakuwa kama dalali katika masoko ya mkulima,"* alisema Mhe. Homera.

Mauzo ya Ufuta kwa Vyama vya Ushirika kupitia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala umewezesha jumla ya kilo 1,370,718 kuuzwa katika minada mitatu (3) iliyofanyika mkoani Katavi msimu huu. Kutokana na mauzo hayo, Shilingi 2,767,200 zililipwa na makampuni yaliyoshiriki kwenye minada hiyo. Kati ya fedha hizo wakulima walilipwa Shilingi 2,555,511,910 kupitia akaunti zao za benki.

Aidha, katika fedha hizo jumla ya Shilingi 82,243,080 zimeingia katika Halmashauri za mkoa wa Katavi kama ushuru ambazo zitatumika katika kuimarisha miradi mbalimbali ya maendeleo katika maeneo hayo.

Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika Mkoa wa Katavi, Kakozi Amri amesema kuwa kumekuwepo na ushirikiano mkubwa katika usimamizi wa Vyama vya Ushirika kati ya viongozi wa mkoa, wilaya, Halmashauri. Ambapo ushikiano huo umewezesha kuongezeka kwa idadi ya vyama, wanchama na idadi ya mazao yanayoshughukiwa na vyama vya ushirika.

"Hapo awali ushirika katika mkoa wa Katavi ulikuwa ukishughulikia zao moja tu la Tumbaku, lakini sasa vyama vya ushirika katika mkoa wetu vinajihusisha pia na mazao ya Pamba, Ufuta, Korosho na Alizeti. Wakulima wameweza kuongeza kipato kutokana na kuuza mazao haya kwa bei nzuri ikilinganishwa na wakati yalikuwa yanauzwa nje ya mfumo wa ushirika," amesema Kakozi.

# CHAMA KIKUU CHA USHIRIKA CHA WAKULIMA (LATCU LTD)




*Mrajis Msaidizi Mkoa wa Katavi, Kakozi Amri (kushoto) akikagua ghala la Chama cha msingi cha Ushirika Ilunde AMCOS lenye uwezo wa kuhifadhi magunia yenye tumbaku 2,000 kwa wakati mmoja*

Chama Kikuu cha Ushirika cha wakulima mkoani Katavi (LATCU Ltd) kilianzishwa mwaka 1994 na mpaka sasa kina vyama vya Ushirika vya msingi wanchama kumi na moja (11) ambavyo ni Mpandakati AMCOS, Nsimbo AMCOS, Katumba AMCOS, Kasokola AMCOS, Majalila AMCOS, Ukonongo AMCOS, Ilunde AMCOS, Mishamo AMCOS, Tanganyika AMCOS, Ilela AMCOS na Utense AMCOS. Aidha vyama vya Kasekese na Kamwendwe vimeomba kujiunga na chama kikuu na vinasubiri kupata ridhaa ya wanachama katika Mkutano Mkuu wa LATCU Ltd.

Chama Kikuu cha Ushirika cha wakulima mkoani Katavi kimekuwa kikiwapatia pembejeo wakulima kupitia vyama vya Ushirika kwa wakati, na kusimamia shughuli za kiuchumi za chama na vyama wanachama wa LATCU Ltd.

Kaimu Meneja Mkuu wa Chama Kikuu cha Ushirika cha wakulima (LATCU Ltd), Fatuma Kombe, amesema kuwa mazao makuu ya biashara mkoani Katavi ni pamoja na Tumbaku ambayo ilianza kuzalishwa mwaka 1970; na mazao mengine ni Pamba na Korosho ambayo yameanza kulimwa mwaka 2018.

*"Tumbaku msimu wa 2018/2019 tumeuza tumbaku kilo 7,144,032 zenye thamani ya USD 10,293,664.41 na Pamba msimu wa 2018/2019 tumeuza kilo 8,562,569.10 zenye thamani ya Tsh. Bilioni kumi milioni mia mbili sabini na tano na themanini na mbili elfu mia nane na kumi na mbili (10,275,082,812/=) msimu wa 2019/2020 tunatarajia kuuza kilo 7,250,000 za Tumbaku na kilo. 13,000,000 za Pamba,"* alisema Kombe.

## Mafanikio ya chama kikuu LATCU Ltd

Chama kikuu kina rasilimali mbalimbali ikiwemo: majengo na ardhi ambayo inategemewa kuendelezwa kwa kujenga majengo ya biashara; vyombo vya usafiri magari (4) na pikipiki 7 kwa ajili ya kazi za chama; na kina Samani na vifaa kwa ajili ya kazi za chama. Aidha, Chama Kikuu kwa kushirikiana na Vyama vya Ushirika wanachanma wa LATCU wameweza kununua gari aina ya Toyota Hilux linalosaidia Ofisi ya Mrajis Msaidizi (M) - Katavi kufanya majukumu ya ushirika.

# Chama cha Msingi cha Ilunde AMCOS

Chama cha msingi cha Ushirika Ilunde AMCOS, kiliandikishwa na kusajiliwa tarehe 28/05/1999 kikiwa na wanachama wapatao 214, hadi sasa chama kina wanachama wapatao 482. Chama hiki kilianzishwa kwa dhumuni moja tu ambalo ni uzalishaji wa zao la tumbaku lakini kwa sasa chama kinajihusisha na mazao mengine kama vile korosho, ufuta, alizeti, mpunga na karanga.

Akizungumzia mafanikio ya Chama cha Msingi cha Ushirika Ilunde Amcos Ltd, Mwenyekiti wa chama hicho, Modesti Yamlinga alisema tangu kuanzishwa kwake kinamiliki mali za aina mbalimbali ikiwemo ofisi ya chama, nyumba ya kulala wageni (guest house), maghala makubwa matatu (3), stoo moja (1), jengo la ofisi (1) na nyumba ndogo ya chama.

*"Mpaka sasa chama chetu kina jumla ya miradi miwili (2) ambayo ni Mradi wa nyumba ya kulala wageni (guest house) na Mradi wa Upangishaji wa maghala,"* alisema Yamlinga.

Kuhusu upandaji miti, Bwana Yamlinga amesema kuwa chama kimekuwa kikifanya hamasa kubwa kwa wakulima wake juu ya upandaji wa miti ili kutunza mazingira kwa ajili ya vizazi vinavyokuja. Chama cha Ilunde AMCOS kinamiliki zaidi ya mashamba manne (4) ya miti na yapo vizuri na kuna mashamba ya mkulima mmoja mmoja. Mafanikio makubwa ya Chama cha Msingi cha Ushirika Ilunde Amcos Ltd ni pamoja na kulipa madeni ya pembejeo na fedha taslimu kwa asilimia 100% licha ya kuwepo na kulipiana ndani ya vikundi vya udhamini; Kuanzisha Mradi wa nyumba ya kulala wageni (guest house); Kujenga maghala makubwa matatu (3) ya kuuzia tumbaku; Kusomesha watumishi wawili kwa masomo ya utawala na uhasibu kwa ngazi ya cheti; Kupokea na kugawa pembejeo kwa wakulima/wanachama; Kusimamia shughuli za masoko vizuri; na Kulipa malipo ya wakulima kwa asilimia 100.

### Chama cha Ushirika cha Msingi Katumba AMCOS

Chama cha Ushirika cha Msingi Katumba AMCOS kiliandikishwa kwenye Daftari la Usajili wa Vyama vya Ushirika Desemba 1995 kikiwa na Wanachama Waanzilishi 120 na hadi sasa Wanachama wameongezeka na kufikia 1,282 na kina wanachama wanaozalisha mazao mbalimbali kwenye kata za Litapunga, Kanoge, Katumba, Mtapenda na Kata ya Urwira.

Katumba AMCOS kilianzishwa kwa lengo la kuwapatia Wanachama nguvu ya pamoja ya uzalishaji wa mazao bora na kuuza kwa pamoja kwenye soko la faida. Pia Wanachama kupitia Ushirika wameweza kupata dhamana na kuweza kukopeshwa na Taasisi za fedha na kuweza kuendesha miradi mingine ya faida kwa Wanachama na Wanajamii kwa ujumla. Katika Utekelezaji wa Mwongozo wa Serikali kwa Vyama na Wanachama wake kuzalisha mazao mchanganyiko na hasa yale ya Kimkakati yanayostawi kwenye maeneo husika ili kuongeza mapato kwa Wanachama na Chama. Katumba AMCOS kilifanya Maboresho ya Masharti yake kutoka Uzalishaji wa zao la Tumbaku na kufanya Wanachama kuzalisha mazao mengine ikiwa ni pamoja na Pamba, Alizeti na Korosho.

**Mali za Chama cha Katumba AMCOS**

Chama cha Ushirika cha Katumba AMCOS kinamiliki Jengo la Ofisi lenye thamani ya Shilingi 113,400,000, Maghala manne (4) yenye thamani ya Shilingi 321,400,000, Gari - Land Cruiser (1) lenye thamani ya Shilingi 62,933,214 na viwanja (4) vyenye thamani ya Shilingi 28,913,250. Mali nyingine ni pamoja na Kompyuta za mezani (4), Kompyuta mpakato (4), Mashine ya photocopy (1), Generator (2), viti, meza na kabati. Vilevile chama kinamiliki mashamba (7) ya miti yenye jumla ya hekari 75.

*"Kwa kutumia udhamini wa vikundi kwenye kilimo cha Tumbaku, usimamizi wa Farm committee na Wajumbe wa Bodi kwenye maeneo wanayosimamia; Chama kinafanikiwa kurejesha mikopoya pembejeo na ya fedha kwa msimu husika. Kwa utaratibu huo, Chama kilifanikiwa kununua mali na samani na Chama kinashiriki kwenyeshughuli za kijamii kwa kutoa michango na huduma katika Elimu na Afya,"* anasema Azory Ntondelo, Mwenyekiti wa Katumba AMCOS.

**Chama cha Ushirika cha Ukonongo AMCOS**

Chama cha msingi Ukonongo AMCOS kimesajiliwa kisheria mwaka 1991 kina jumla ya wanachama 1,691 na katika msimu wa Kilimo 2018/2019 kina idadi ya vikundi vipatavyo 251 ambapo kila kikundi kina idadi ya wakulima wasiozidi kumi (10); vikundi hivi husaidia Wakulima kudhaminiana ili kuweza kupata Pembejeo za Kilimo.

Chama cha msingi Ukonongo kilianzishwa kwa madhumuni ya kushughulika na kilimo cha zao la Tumbaku pekee lakini kutokana na mabadiliko ya masharti ya Chama yaliyofanyiwa marekebisho mwaka 2017 ambayo yamepelekea Chama cha msingi Ukonongo kujishughulisha na mazao mchanganyiko. Kutokana na mabadiliko hayo, Chama kinaendesha shughuli za Kilimo cha mazao ya biashara na chakula hususani Tumbaku, Mahindi, Mpunga, Karanga, Alizeti, Ufuta na Korosho kwa Wanachama.

Hadi hivi sasa Chama cha msingi Ukonongo kinaendelea na utekelezaji wa agizo la Serikali la kuanzishwa mfumo wa stakabadhi ghalani kwa mazao ya Alizeti na Ufuta. Pia Chama kinaendeleza shughuli nyingine za kiuchumi kama: Kuendeleza elimu ya Ushirika kwa Wanachama; Kukusanya, kutafuta masoko na kuuza mazao ya Wanachama; na Kununua, kuhifadhi na kuuza zana za kilimo pamoja na Pembejeo. Akizungumzia kuhusu mali za chama cha msingi Ukonongo AMCOS, Mwenyekiti wa chama hicho, Malilo Godfrey alisema kuwa chama kinamiliki jengo la biashara (18,750,000/=), ofisi ya chama (13,997,184/=), Jengo jipya la chama (43,675,000/=), ukumbi wa chama (57,807,274/=), gari – Scania 93 (33,000,000/=) na maghala 11 yenye thamani ya Shilingi 410,000,000.

*"Chama chetu cha Ukonongo AMCOS kimefanikiwa katika nyanja mbalimbali ikiwemo: Kuwalipa Watumishi wake mishahara kwa wakati; kuboresha zaidi Kilimo cha zao la Tumbaku na kimeendelea kusimamia shughuli za masoko na malipo ya Tumbaku; kuendesha semina kwa watendaji na Wajumbe ili kuwajengea uwezo wa utendaji wa kazi za Chama; na kuboresha mahusiano mazuri na wadau wake kama vile Premium Active (T) LTD, Bodi ya Tumbaku, Mabenki na Chama Kikuu LATCU LTD,"* alisema Malilo.

**Chama cha Ushirika cha Mazao Kasokola AMCOS**

Chama cha Ushirika cha Mazao Mchanganyiko cha Kasokola AMCOS kilianzishwa mwaka 2014 chini ya Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya Mwaka 2013 kikiwa na wanachama 332. Hadi sasa idadi ya wanachama wameongezeka na kufikia 409 na kinahudumia vijiji nane (8) ambavyo ni Manga, Shankara, Kasokola, Itenka, Majalila, Nsanda, Kasolwa na Ivungwe.

*"Chama chetu tangu kianzishwe kimekuwa kikishughulika na zao la Tumbaku, mpaka kufikia mwaka 2018 tulianza kuwahudumia wakulima wa Pamba na kuongezeka kwa mazao ya Ufuta na Alizeti kwa msimu wa 2019/2020,"* alisema Jonas Msusa, Mwenyekiti wa Kasokola AMCOS. Chama cha Ushirika cha Kasokola AMCOS kina jengo lenye thamani ya Shilingi 59,705,000 ambazo ni ushuru uliotokana na zidio la uzalishaji msimu wa 2016/2017 pamoja na michango ya Wanachama. Aidha, chama kina shamba la hekari 15 ambazo hekari 4 zimepandwa miti 19,110 ambayo ni mali ya wanachama.

Kasokola AMCOS kimepata mafanikio makubwa t angu kuanzishwa kwake, mafanikio hayo ni pamoja na: kukopa mikopo ya pembejeo na Cash Advance kwa misimu Mitano (5) na kurejesha mikopo hiyo kwa asilimia 100 kila msimu;

kupata jengo la ofisi lenye thamani ya Shilingi 59,705,000; kuwa na shamba la miti la hekari 15 lenye thamani ya Shilingi 5,800,000; kutoa ajira za kudumu na mikataba kwa wakazi wa eneo husika; kujenga majiko ya kisasa na mabani na kuwezesha wanachama kuwa na mashamba ya pamoja ya miti kwa kila kijiji; na chama kimeongeza mazao mengine kama Pamba, Alizeti na Ufuta.




*Makao makuu ya Chama Kikuu cha Ushirika cha wakulima mkoani Katavi (LATCU Ltd)*

Together We Build Our Economy

# HEIFER INTERNATIONAL YATOA GARI NA CANS KWA VYAMA VYA USHIRIKA WA WAFUGAJI MKOANI TANGA




*Naibu WazirIwa Mifugo na Uvuvi, Mhe. Abdallah Ulega akiwa na Wanaushirika mbele ya gari la ukusanyaji wa maziwa kutoka kwa vyama vya msingi vya wafugaji hadi kiwandani Tanga Fresh Ltd kwaajili ya Usindikaji.*

Chama Kikuu cha Ushirika wa Wafugaji mkoani Tanga – Tanga Diary Cooperative Union (TDCU) na Vyama vyama vya Ushirika wanachama wa chama hicho wamepewa gari na cans na Shirika la Kimataifa lisilokuwa la Kiserikali Heifer International kupitia program zake za kusaidia ukusanyaji wa maziwa kutoka kwa vyama vya msingi vya wafugaji.

Gari lililotolewa litasaidia ukusanyaji wa maziwa kutoka kwa vyama vya msingi vya wafugaji hadi kiwandani Tanga Fresh Ltd kwa Usindikaji ambapo cans zilizotolewa zitagawanya kwa vyama vya msingi wanachama wa TDCU na gari litakuwa linachukua maziwa katika vyama vyote vya ushirika.

Cansna gari vilikabidhiwa kwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mhe. Abdallah Ulegana Bw. Mac wa Heifer International alipotembelea Vyama vya Ushirika wa Wafugaji wa ng'ombe wa maziwa katika wilaya ya Muheza mkoani Tanga ambapo alikabidhiwa vibebea maziwa (cans) 50. Gari lililokabidhiwa kwa TDCU linauwezo wa kubeba lita 15,000 kwa mara moja na lina thamani ya Shilingi 170 milioni.Heifer International wameamua kutoa gari jingine kufika mwezi Novemba,2020 baada ya kuona usimamizi mzuri wa gari la kwanza.

Aidha, Naibu Waziri Ulega katika ziara hiyo alijionea mafanikio na changamoto za mkopo wa TADB kwa wafugaji wa mkoa wa Tanga kwa kuwa mkoa huo ndio ulikuwa wa majaribio (pilot) kwa mikopo ya TADB kwa Sekta ya Ufugaji. Kutokana na changamoto alizojionea, Mhe. Ulega alielekeza Wataalam wa Sekta Binafsi kukaa na TADB kutoa mwelekeo wa nini kifanyike kwa Wafugaji waliopata hasara kutokana na ng'ombe walikopeshwa kutokutoa maziwa.



*Naibu Wazir wa Mifugo na Uvuvi, Mhe. Abdallah Ulega akikabidhi vibebea maziwa (cans) 50 kwa Wanaushirika wa Chama Kikuu cha wafugaji Mkoani Tanga (TDCU) kwa ajili ya ubebaji maziwa*




*Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mhe. Abdallah Ulega akikabidhiwa gari la kubebea maziwa na Bw. Mac wa Heifer International kupitia program zake kusaidia ukusanyaji wa maziwa kutoka kwa vyama vya msingi vya wafugaji hadi kiwandani Tanga Fresh Ltd kwa Usindikaji.*

# USHIRIKA WA NYUMBA KUWAWEZESHA WANANCHI KUPATA NYUMBA BORA



*Wajumbe wa Kikao katika picha na Wajumbe wa Sejeseje HCS*

Nyumba ni moja ya mahitaji muhimu ambayo kila binadamu anahitaji ili aweze kuishi akiwa na afya njema na kumpatia hifadhi yenye usalama. Kuishi katika nyumba bora humfanya mtu awe na afya njema na humwezesha atoe mchango mkubwa katika shughuli za uzalishaji mali. Uhamiaji wa watu wengi kutoka katika maeneo ya vijijini kwenda mijini umesababisha kuongezeka kwa matatizo ya nyumba hasa maeneo ya mijini. Kwa kuzingatia hili, vyama vya ushirika wa nyumba vimepewa msukumo mkubwa ili kuwezesha wananchi kupata nyumba bora na kupunguza matatizo ya nyumba hasa maeneo ya mijini.

Mratibu wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi - Tawi la Dodoma, Bahati Rukiko, anasema kuwa Vyama vya ushirika wa nyumba ni njia muhimu ya kuwawezesha wananchi wa kipato cha chini kupata nyumba bora kwa gharama nafuu na kuhakikisha uwepo wa usimamizi thabiti wa maeneo ya makazi. *"Pamoja na kuwa na umuhimu mkubwa, ukuaji wake umekuwa ni mdogo sana ikilinganishwa na vyama vya ushirika katika sekta nyingine. Jitihada mbalimbali zimeendelea kufanyika katika kuhamasisha ushirika wa nyumba nchi. Moja ya jitihada hizo ni mkutano wa Wadau wa Ushirika wa Nyumba nchi uliofanyika katika ukumbi wa Karimjee Jijini Dar- es -Salaam tarehe 02 Oktoba, 2017 ambapo pamoja na mambo mengine wanaushirika wa Nyumba waliamua kwa kauli moja kuanzisha Chama Kikuu cha Ushirika wa Nyumba na kuchangua kamati maalumu yenye wajumbe saba (7) ili kuwezesha uanzilishi wa*

*Chama hicho,"* amesema Rukiko.

Baada ya mkutano wa Karimjee, kamati ya uanzilishi inayoongozwa na Hilari Mdaki imendelea kufanya uhakiki wa Vyama vya Ushirika wa Nyumba nchini ambapo hadi sasa uhakiki umefanyika kwa vyama 12 katika mikoa ya Kagera, Mwanza, Mara, Shinyanga, Dodoma na Iringa. Hata hivyo zoezi hilo halikuweza kukamilika katika Mikoa mingine baada ya kukosa fedha za kuendelea na kazi hiyo. Kutokana na hali hiyo, Wataaalmu wahamasishaji wa Vyama vya Ushrika wa Nyumba kutoka Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania ( TCDC), Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi- Ofisi ya Dodoma na Kampuni ya CPM Land Developers ya Jijini Dar es Salaam walifanya kikao kazi cha siku mbili kuanzia tarehe 29/06/2020hadi 30/06/2020 Ofisi ya Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU) -Dodoma ili kujadili changamoto za Ushirika wa Nyumba na kuweza kutayarisha mpango wa kuhamasisha na kuendeleza Ushirika katika sekta ya Nyumba. Katika kikao hicho wajumbe walipitia utekelezaji wa maazio ya mkutano wa Wadau wa Ushirika wa Nyumba wa Mwaka 2017, kupitia taarifa ya uhakiki wa vyama vya Nyumba kujaadili mifumo ya upatikanaji wa fedha kwa Vyama vya Nyumba zilizokuwa zimeandaliwa na Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi - Ofisi ya Dodoma.

Kupitia kikao hicho cha siku mbili, Wajumbe walipata fursa ya kutembelea Chama cha Ushirika wa Nyumba Sejeseje kilichopo katika eneo la Miyuji Jijini Dodoma ili kuona maendeleo ya chama hicho na changamoto zinazokibabili na hatimaye kubaini njia za utatuzi wa Changamoto hizo. Wajumbe walikutana na Mwenyekiti wa Chama hicho, Katibu na Mkurugenzi wa Shirika la Centre for Community Initiative (CCI), Dkt. Tim Ndezi ambao ndiyo waliwezesha unazishwaji wa chama hicho. Wajumbe walibaini kwamba kwamba vyama vingi vya Ushirika wa Nyumba havifahamiki na Mamlaka za usimamaizi wa Vyama vya Ushirika na kwa sababu hiyo vimekuwa vikikosa usimamizi wa kutosha. Vyama vingi haviwasilishi makisio ya mapato na matumizi kabla ya kuanza mwaka wa fedha na pia havifanyi ukaguzi wa hesabu za fedha. Pia ilioneka na kwamba vyama vya ushirika wa nyumba kwa muda mrefu havijafanya uchaguzi wa viongozi wa Bodi za Uongozi kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya Mwaka 2013. Hata vyama vingi vimekuwa vikianzishwa lakini vimekuwa vikishindwa kujenga nyumba za wanachama kutokana na kukosa fedha za kuwezesha ujenzi wa nyumba.Kwa sababu hiyo, wajumbe walijadili mifumo ya namna ya kuwezesha upatikanji wa fedha kwa Vyama vya Ushirika wa Nyumba ambapo mifumo iliyojadiliwa ni Mfadhiri- Mjenzi **(Funder – Builder Financing Approach )** na Mfuko wa Ujenzi wa Nyumba **( Solidarity Housing Development Fund).**




*Wajumbe nje ya Ofisi ya Sejeseje H.C*

TCDC
Together We Build
Our Economy

TANZANIA CO-OPERATIVE DEVELOPMENT COMMISSION

**TCDC**

**Together We Build Our Economy**